Mfano wa Barua ya Kuthibitisha
Inayochapishwa kwenye Anwani ya Mtoa Huduma za Afya

(Sehemu ya I)

Tarehe:

Mpendwa Mtoa Huduma za Nyumba:

Nimekuwa _____ [mshauri, muuguzi, daktari, tabibu, daktari wa magonjwa ya akili] wa Name tangu _____.

Ninafahamu kuwa Sheria ya Nyumba za Bei Nafuu (Fair Housing Act) na Kifungu cha 504 cha Sheria ya Urekebishaji wa Tabia (Rehabilitation Act) kinafafanua ulemavu kama:

1. Tatizo la kimwili au kiakili ambalo linaathiri kwa kiwango kikubwa shughuli moja au zaidi kuu za maisha ya mtu, na/au
2. Rekodi ya kuwa na tatizo la kimwili au kiakili ambalo linaathiri kwa kiwango kikubwa shughuli moja au zaidi kuu za maisha ya mtu, na/au
3. Kuchukuliwa kama mtu aliye na tatizo la kimwili au kiakili ambalo linaathiri kwa kiwango kikubwa shughuli moja au zaidi kuu za maisha ya mtu.

Shughuli kuu za maisha ni pamoja na, wala si tu: uwezo wa kujitunza, kufanya kazi za mikono, kutembea, kuona, kusikia, kuzungumza, kupumua, kusoma, na/au kufanya kazi.

Ninathibitisha kuwa Name ana ulemavu ambao unatimiza ufafanuzi huu wa kisheria.

(Sehemu ya II)

Name ana ulemavu ambao UNAHITAJI *** mnyama msaidizi** (paka, anayeitwa: Toby) .

Ni MUHIMU Name aruhusiwe kuwa na *** mnyama msaidizi** nyumbani kwake haraka iwezekanavyo ili tatizo la ulemavu la ____Name____ litatuliwe, lisiongezeke na/au kuwa baya zaidi.

Wako mwaminifu,
[Daktari, Muuguzi, Msaidizi wa Daktari, Tabibu/Mshauri, Mtoa Huduma za Jamii, Daktari wa Magonjwa ya Akili, Mtaalamu wa Maisha ya Kujitegemea, nk.]

Maelezo ya mawasiliano ya Mtoa Huduma za Afya

***Mifano ya RA:** nafasi ya maegesho iliyotengwa, kuongezwa kwa muda wa mkataba wa kukodisha nyumba, kusimamishwa kwa mkataba wa kukodisha nyumba bila adhabu, kuhamia kwenye vyumba vingine, kutuma kodi ya nyumba kwa njia ya barua, nk.

***Mifano ya RM:** kuweka chuma ya kushikilia au lifti, kubadilisha vishikio vya mlango vya duara na kuweka vishikio paba, kupunguza urefu wa vitu, kupanua mlango, kuweka sakafu ya kuteremka kwenye bafu, nk. **Ni Nani Anayelipa?** Marekebisho mara nyingi huwa na gharama ambayo ni hugharamiwa na mtu mwenye ulemavu isipokuwa awe anaisha kwenye nyumba ya bei nafuu ya serikali. Inapandekezwa sana kurekodi ombi la kufanywa kwa marekebisho na matarajio mwishoni mwa mkataba wa kukodisha nyumbani kuhusu kurejesha nyumba katika hali yake ya kawaida.

Ni nani anayeelezwa kama “Mtu mwenye Ulemavu”?

Chini ya Sheria ya Nyumba za Bei Nafuu (Fair Housing Act), ulemavu unafafanuliwa kama:

- Tatizo la kimwili au kiakili ambalo linaathiri kwa kiwango kikubwa shughuli moja au zaidi kuu za maisha
- Rekodi ya tatizo kama hilo, au,
- Kuchukuliwa kama mtu aliye na tatizo kama hilo.

Chini ya RCW 49.60, Sheria ya Jimbo la Washington Inayopinga Ubaguzi, (Washington State Law Against Discrimination, WLAD), ulemavu umefafanuliwa ili kujumuisha hali ambazo ni za muda mfupi au za kudumu, za kawaida au zisizo za kawaida, zinazoweza kusuluhishwa au zisizoweza kusuluhishwa.

EQUAL HOUSING OPPORTUNITY

Ikiwa unafikiri kuwa umebaguliwa katika shughuli ya kutafuta nyumba, wasiliana na:

Northwest Fair Housing Alliance
25 W Main Ave., Suite 250
Spokane, WA 99201
509-325-2665
1-800-200– FAIR (3247)
Faksi: 1-866-6308

NWFHA inaweza kukushauri kuhusu chaguo ulizo nazo na kukutetea. Huduma zetu ni za bure. Ofisi yetu iko wazi kwa kila mtu.

Kazi iliyotoa msingi wa kuchapishwa kwa chapisho hili iliungwa mkono kwa sehemu fulani kwa ufadhili chini ya ruzuku kutoka kwa Wizara ya Nyumba na Maendeleo ya Miji ya Marekani (U.S. Department of Housing and Urban, HUD). NWFHA inawajibika kikamilifu kwa usahihi wa taarifa na ufafanuzi ulio kwenye chapisho hili.
Kiingereza– 8/2021– SWAHILI

Sheria ya Nchi ya Nyumba za Bei Nafuu

Wanyama Wasaidizi katika Makazi

Mwongozo wa Watu wenye Ulemavu

NORTHWEST FAIR HOUSING ALLIANCE

(509) 325-2665
1-800-200-FAIR (3247)
www.nwfairhouse.org

Makazi Yanayofaa (RA) :

kubadilishwa, kutengwa au kurekebishwa kwa sheria, sera, utaratibu au huduma ambayo inaruhusu mtu mwenye ulemavu kutumia na kufurahia nyumba, ikiwa ni pamoja na maeneo ya umma. Kuwa na mnyama msaidizi katika nyumba "zisizoruhusu wanyama vipendwa" ni mfano wa RA.

Jamii, Ukubwa, Uzito, Spishi

Sheria za mtoa huduma za nyumba kuhusu spishi za wanyama vipendwa, ukubwa, uzito na jamii hazitumiki kwa wanyama wasaidizi. Hata hivyo, idadi na spishi za wanyama wanaoruhusiwa zinaweza kudhibitiwa na sheria za manispaa yako (k.m., vikomo vya idadi ya wanyama wanaofugwa nyumbani, kupigwa marufuku kwa mbwa mwitu na nyoka wenye sumu kali, nk.)

Wanyama Wasaidizi

Wamiliki huita wanyama "majina" tofauti kwa ajili ya kwa mfano: tiba, msaada wa kihisia, dawa, kuarifu kuhusu matibabu, rafiki, kutembea, tiba ya ugonjwa wa akili, mnyama wa kutoa huduma, mbwa wa kuongoza, nk. Lakini jina si hoja.
Ili kuruhusiwa katika mpango wa makazi yanayofaa, lazima mnyama **ahitajike kwa ajili ya ulemavu**.
Watu wenye aina mbalimbali ya ulemavu unaoonekana na usioonekana (kimwili au kiakili) hutumia wanyama wasaidizi: kuleta dawa, kuashiria kutokea kwa hali ya kifafa, kuarifu kuhusu kuhitaji dawa ya insulini, kutuliza wasiwasi, kupunguza Msongo wa Mawazo. Wasiwasi au PTSD, kuitikia na kuarifu mtu ambaye ni kiziwi au mwenye matatizo ya kusikia, kuongoza na kuelekeza watu ambao ni vipofu, nk.

Majukumu ya Mmiliki:

- Zoa na utupe ipasavyo uchafu wa mnyama
- Dhibiti mnyama kila wakati, kwa kawaida hii inamaanisha kwa kutumia ukanda
- Tabia ya mnyama: hapaswi kukimbilia mtu, kurukia, kuuma, kunyofoa au kubweka zaidi
- Anapaswa kuwa na leseni, kuchanjwa, kusajiliwa kama inavyohitajika na mji/jiji ambapo unaisha

Utatuzi: suluhu

- Mavi / uchafu — mlezi/rafiki/mwanafamilia anaweza kusaidia kuzoa uchafu na kuutupa ipasavyo kwa ajili ya mtu mwenye ulemavu
- Kunyofoa/kuuma — tumia kifungo cha mdomo unapoingia na kuondoka kwenye jengo au unapoenda katika maeneo ya umma kama vile lifti au chumba cha dobi
- Kubweka zaidi — mafunzo ya utiifu na ushughulikiaji
- Kukimbia huru—mafunzo ya ziada ya kudhibiti kwa sauti na/au matumizi ya ukanda kila wakati

Je, kuna ada? Je, kuna fidia? Je, Vyeti vya Wanyama vinahitajika?

- **Amana za Mnyama Kipendwa, Ada,** Wanyama wasaidizi wa kukodisha si "wanyama vipendwa" kwa hivyo ada za mnyama kipendwa, kodi, amana lazima ziondolewe
- **Fidia:** Mmiliki wa mnyama anawajibika kwa uharibifu unaosababishwa na mnyama msaidizi na anaweza kutozwa gharama za ukarabati au ubadilishaji wakati au baada ya mkataba wa kukodisha nyumba kuisha
- **Vyeti vya Wanyama:** "Kitambulisho" cha mnyama hakihitajiki. Ni mmiliki wa mnyama anayezingatiwa:
  1.) lazima mtu awe na ulemavu 2.) hitaji la ulemavu linalohitaji mnyama huyo lazima libainishwe 3.) lazima mnyama awe anafaa

Kuomba Mnyama Msaidizi

- Mtu mwenye ulemavu au mwakilishi wake (*rafiki, famila, shirika la utetezi*) anaweza kutuma ombi. Hakuna aina au muundo maalum unaopaswa kutumiwa kutuma maombi.
- Maombi yanaweza kutumwa kwa kutamka. Kwa uwazi, ***inapandekezwa sana kuwa maombi yatumwe kwa njia ya maandishi.*** Baki na nakala.
- Ombi halihitaji kufichua hali au ukali wa ulemavu wa mtu, na watoa huduma za nyumba hawawezi kuuliza kuhusu hali hizi.
- Ni muhimu kuonyesha hitaji linalohusiana moja kwa moja na ulemavu.
- Mtu anayeoomba mnyama msaidizi anaweza kuulizwa atoe **barua ya kuthibitisha** kutoka kwa mtoa huduma za afya au mtu mwingine wa kutegemewa ambaye anafahamu ulemavu wa mtu huyo (mfano unapatikana nyuma.)
- Ulemavu wa wazi, unaoonekana au unaojulikana **hauhitaji** kuthibitishwa kwa ulemavu—lakini unaweza kuhitaji kuthibitisha **hitaji linalohusiana** na ulemavu ikiwa si ulemavu wa wazi au unaojulikana.
- Maombi ya RA yanaweza kutumwa wakati wowote katika kipindi cha mkataba wa kukodisha nyumba (unaweza kutuma maombi hadi wakati wa kukomeshwa kwa mkataba/kufurushwa).
- Hakuna kikomo kwa idadi ya maombi ya RA ambayo mtu anaweza kutuma.